SOMO LA TATU



YESU ALIKUWAJE?

Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.

HAKUWA NA DHAMBI KABISA



Maisha ya haki yaliyo imara

Mtu ambaye Mungu alimchagua kuhukuu mawazo, maneno, na matendo ya watu ni lazima awe asiye na dhambi. Kila kitu tunachokijua juu ya Yesu kinauonyesha ukamilifu Wake.[1] Maisha yake yalikuwa manyofu kama kamba ya fundi (kabiro) na kipimo cha haki (wema) tupaswao kuwa nao.

Katika somo hili tutaona jinsi Yesu alivyoishi maisha ya kiwango cha juu zaidi hata ya mafundisho Yake Mwenyewe. Hili linaufanya usemi Wake wa kuwa Hakimu wa dunia anayefaa ndiye pekee (somo la 2). Lakini pia ina maana Yesu ndiye afaaye na kustahili/anayejali na mwenye huruma, siyo kwa wagonjwa tu ila pia na kwa wenye dhambi!

YOHANA MBATIZAJI ALIJUA KUWA YESU HAKUWA NA DHAMBI

Yohana alikuja kuandaa watu kwa ajili ya Yesu, na kuwabatiza wale waliogeuka kuachana na dhambi zao. Alisema hakustahili hata kulegeza kamba za viatu vya Yesu. Hii haikuwa kwa sababu Yohana alikuwa mtu mbaya, lakini ni kwa sababu Yesu alikuwa ni mtu mwema.
Angalia juu katika Marko 1:7

Kumbukumbu ya Kihistoria:
Yohana mbatizaji alionekana tofauti kwa Yesu. Alivaa nguo ngumu na alikula nzige na asali ya mwituni.

.....

.....

.....

Yohana hakutaka ambatize Yesu, maana alijua Hakuwa na dhambi za kuachana nazo.[2]

MUNGU ALIMTANGAZA YESU KUWA ASIYE NA DHAMBI

Yesu ni mtu pekee kati ya wote aliyempendeza Mungu. Hakuna mwingine aliyetangazwa hadharani kutoka mbinguni kuwa alimpendeza Mungu. Yesu alipobatizwa, Mungu kwa wazi kabisa alitangaza kuwa Yeye alipendezwa na Yesu. Angalia Marko 1:11

Yesu pekee ndiye aliyempendeza Mungu kwa hakika

.....

.....

Mungu baadaye alitoa tangazo linalofanana juu ya Mwanaye.[3] Mtu ni lazima awe msafi (mtakatifu) ili kumpendeza Mungu aliye mtakatifu!

[1] 1 Yohana 3:5.
[2] Mathayo 3:13-14.
[3] Mathayo 17:5.

WAANDISHI WA AGANO JIPYA WALISEMA YESU HAKUWA NA DHAMBI

Hakuwahi kuangukia katika jaribu

Yesu alijua nguvu za majaribu lakini hakutoa nafasi kwayo. Kama angelitoa nafasi, basi angekuwa mwenye dhambi kama sisi. Angalia Waebrania 4:15

.....

.....

.....

Utimilifu/ustahilivu wa Yesu ulionyesha kutostahili kwa wengine. Hata Petro (mwanafunzi Wake) aligundua na kuhisi nguvu za kushindwa na dhambi mbele za Yesu.[4] Yesu "hakuijua wala hakuwa na dhambi." [5] Angalia ushahidi/mifano ya hili katika maisha Yake yaliyofuata.

Mkono wa upendo

ALIISHI SAWASAWA NA MAFUNDISHO YAKE

Unakumbuka jinsi Yesu alivyosema kuwa tunatakiwa kumpenda Mungu na kupendana? Alsisema tunapaswa kuwapenda wengine kama tunavyojipenda.[6] Pia alisema tunatakiwa kuwapenda maadui zetu – kitu kigumu kati ya vyote vya kufanya! Japo kiwango hiki ni kigumu/hakiwezekani kwetu, Yesu aliweza kufanya hivyo!

YESU ALIMPENDA MUNGU KWA UBINADAMU WAKE WOTE

Wazo la mateso lilipomfunika na kumzidia Yesu, aliyaacha mapenzi Yake mikononi mwa mapenzi ya Baba Yake wa Mbinguni. Angalia Luka 22:42

.....

.....

.....

YESU ALIWAPENDA WENGINE KAMA ALIVYOJIPENDA MWENYEWE

Alifikiri tu juu ya wengine

Yesu hakuwa na ubinafsi kabisa. Alipokuwa anakufa msalabani, Yesu alifikiri juu yaw engine na siyo Yeye mwenyewe. Japo katika mateso makali alifikiri juu ya mamaye, na akamwomba mwanafunzi amtunze.
Soma Yohana 19:26-27. Andika mstari wa 27

.....

.....

.....

YESU ALIWAPENDA MAADUI ZAKE

Jinsi gani ilivyo vigumu kuwapenda rafiki zetu!

Walipokuwa wakifanya maovu ya kumuumiza msalabani, Yesu alimwomba Mungu awasamehe – kitu ambacho Alikuwa tayari kukifanya Mwenyewe. Angalia Luka 23:34

.....

.....

.....

[4] Luka 5:8. Alisema "Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana!"
[5] 2 Wakorintho 5:21.
[6] Mathayo 22:39.

ALIJAA HURUMA



Jinsi gani alivyowaendea wagonjwa

Miujiza mingi aliyoifanya Yesu ilikuwa yenye huruma, kama tulivyoona katika (somo la 1). Moyo Wake wa huruma uliwaelekea wengine katika mahitaji yao, na aliwaponya.

ALIITUMIA HURUMA YAKE KWA WENGI

Yesu alikuja kuhubiri Injili. Lakini eneo la watu wengi wagonjwa lilimgusa zaidi, hivyo aliwaponya wote walioletwa Kwake.[7] Angalia Mathayo 14:14

.....

.....

.....

ALIITUMIA HURUMA YAKE KWA WAWILI TU

Aliwapa kuona vipofu

Watu vipofu mara kwa mara walilazimika kuombaomba ili waweze kuishi/kula. Mateso yao yaliugusa moyo wa Yesu na kumsukuma kuwahurumia. Angalia Mathayo 20:34

.....

.....

.....

Kuna mifano mingine mingi inayoonyesha huruma ya Yesu kwa wagonjwa. Pia aliwaonea huruma wenye njaa[8] na watesekao/wenye huzuni.[9]

ALIJAWA NA HURUMA KWA WENYE DHAMBI

Jaribu ni kama upepo mkali

Fikiri juu ya u pepowenye nguvu ambao ni vigumu kutulia. Hii ni picha ya majaribu. Majaribu ni kama upepo wenye nguvu. Yesu alijua nguvu za majaribu, na shida ambayo dhambi humpelekea mtu. Pamoja na kuwa Yesu Mwenyewe hajawahi kutenda dhambi, aliwahurumia wale waliotenda dhambi.

Yesu alikula pamoja na baadhi ya watu wabaya walioishi siku Zake. Baadhi walimlaumu kwa kuwa na mahusiano na wenye dhambi, lakini walishindwa kugundua kuwa wao walikuwa wenye dhambi wenyewe.[10]

YESU ALIENDA KWA WENYE DHAMBI

Ni kwa sababu Yesu alikuwa mwenye haki kwamba Aliwapenda wenye dhambi kuliko tunavyoweza, au tunavyofanya. Yesu alikosolewa kwa kuwakaribisha wenye dhambi. Angalia Luka 15:2

Upendo wa kweli

.....

.....

.....

[7] Mathayo 4:23-24 na 8:16-17

[8] Marko 8:2-3.

[9] Mathayo 9:36, na soma Luka 7:11-15 kwa mfano mwingine wa huruma ya Yesu.

[10] Mathayo 11:19.

Aliwapenda wenye dhambi, siyo dhambi

Ni kwa sababu Yesu alijua dhambi ingeharibu maisha na kuwateketeza watu ndiyo maana Aliwapenda wenye dhambi sana. Pia alijua kuwa dhambi ingewatenga na mbingu. Alikuwa na upendo mwingi kwa wenye dhambi au kama Biblia inavyosema, "mwingi wa neema". Angalia Yohana 1:14

.....

.....

.....

.....

WENYE DHAMBI WALIJISIKIA KUMWENDEA YESU

Aliwapenda wasiopendwa.

Wale waliogundua dhambi zao walimwendea kwa sababu waliuhisi upendo Wake kwao. Soma Luka 7:37-38. Andika mstari wa 37

.....

.....

.....

.....

Tumeona mwanzoni kuwa Yesu alikuja kuwaokoa wale "waliopotea" (somo la 2). Nukuu hapo chini inatoa mifano mingi ya wenye dhambi waliookolewa na Yesu.[11]

NA MWISHO

Hatuwezi kumaliza somo hili lenye sifa za Yesu bila kutaja ujasiri Wake. Katika sehemu zenye upinzani mkubwa, aliukabili bila upendeleo. Hii nayo ni sehemu nyingine ya haki Yake. Mtu mwenye uoga na kujiuzulu/kukata tamaa hawezi kuwa mwenye haki.

Yesu hakuwa na upendeleo

Yesu alionyesha ujasiri mkubwa alipowakemea watawala wa nyakati Zake,[12] kuwafukuza nje wale waliolitukana hekalu la Mungu,[13] na kwa jinsi alivyosimama kwa utulivu/unyenyekevu katika utawala wa Rumi alipokuwa akishtakiwa.[14]

Maonyo/kutokubaliana na mamlaka ilikuwa ni moja ya sababu, usemi wa kibinadamu, kwa ajili ya kifo Chake (somo lifuatalo).

[11] Mathayo (Mathayo 9:9-13); Zakayo (Luka 19:1-10); mwizi aliyekuwa anakufa (Luka 23:39-43).
[12] Luka 11:42-54.
[13] Marko 11:15-19.
[14] Yohana 19:5-11